



KITUO CHA ZANA ZA MAWE ISIMILA





Utangulizi

Isimila ni moja kati ya vituo vya malikale yenye historia ya kale kuhusiana na utamaduni wa mtu wa kale juu ya ufundi wa kutengeneza na kutumia zana za mawe yapata miaka milioni 1.6 iliyopita.

Bonde hili la Isimila zinapatikana zana za mawe za mihula tofauti nyingi zikiwa ni za jamii ya Ashilian (Acheulian).

Hifadhi hii ya malikale ya Isimila ni ya kipekee kwa sababu ya uwepo wa zana nyingi za mawe kuliko sehemu yoyote duniani. Hii inaonyesha kuwa kulikuwa na maisha ya binadamu wa kale katika eneo hili, ambao waliishi kwa kipindi kirefu.

Historia ya kituo

Neno Isimila limetokana na neno la Kihehe Pepisimike likimaanisha makazi ya kudumu.



Eneo la kituo cha Zana za mawe Isimila ni la kihistoria ikihusisha ugunduzi wa zana za mawe katika korongo la Isimila uliofanywa na Bwana D.A Maclean wa Afrika Kusini na Amin Azan Mturi (Mtanzania) mwaka 1951. Pia katika uchimbuzi wa mwaka 1957 uliofanywa na watafiti kutoka Chuo kikuu cha Chicago na uchimbuzi wa mwaka 1969 uliofanywa na watafiti kutoka chuo kikuu cha Illinois vyote vya Marekani. Tafiti hizi zilionesha uwepo wa Zana za kale za mawe katika bonde la Isimila.



Eneo la bonde la Isimila lina makorongo mawili moja zinapatikana zana za mawe na lingine zinapatikana nguzo za asili zenye tabaka la miamba ya rangi tofauti.

Jinsi ya kufika

Eneo la Makumbusho ya Isimila linapatikana kusini mwa mji wa Iringa Km 21 barabara ya kuelekea Mbeya. Kutokea Iringa mjini panda gari zinazoelekea Tanangozi, Ifunda au Mafinga, shuka kituo cha Isimila kibaoni.

Bidhaa za Kitalii

Shughuli za kitalii ni pamoja na kutembea kwenye bonde la zana za mawe na nguzo asili, kupiga picha, kuangalia ndege hasa kabla ya msimu wa baridi kuanzia Juni hadi Septemba na Utalii wa michezo Vivutio vilivyopo ni pamoja na mabonde mazuri yenye mandhari na



historia ya kale, zana za mawe, nguzo za asili, makumbusho, kituo kina eneo zuri la kuweka kambi za muda.

Pia kituo hiki kimeweza kutunza zana mbalimbali ambazo zilitumika na makabila ambayo yanapatikana kusini mwa Tanzania hasa kwa makabila kama Wahehe na Wabena ambayo yalikuwa na makazi yake katika mkoa wa Iringa.

Pia eneo hili ni zuri kwa ajili ya shughuli za utafiti wakiakiolojia na jiolojia

Sehemu nzuri ya wanafunzi kujifunza (study Tour)

Kituo kinawakaribisha watazania wote kuja na kutembelea kituo hiki ili kujionea na kujifunza historia mbalimbali za enzi za zama za mawe.





TOZO

Lake
Eyasi

Raia wa Afrika Mashariki (TShs)	Wasio Raia wa Afrika Mashariki (USD)	Wageni wakazi (USD)
2000	10	5
1000	5	2.5
Bure	Bure	Bure

Miaka 16 na zaidi

Miaka kati ya 5 hadi 16

Chini ya miaka 5

Malipo haya bila VAT

Malipo yote ya viingilio yanafanyika kwa kutumia mtandao bank, Mpesa, Tigo Pesa, AirtelMoney n.k

Siku za kazi

J-tatu-Ijumaa


Wikiendi - Sikukuu

Muda

Saa 2:00 Asubuhi-11:30 Jioni

Saa 2:00 asubuhi-11:00 Jioni





AFTER HALDEMAN

Kwa Mawasiliano zaidi:

Kituo cha Zana za Mawe-Isimila

S.L.P. 369

Isimila - Iringa, Tanzania

Simu: +255 26 2965845.

Baruapepe: ismila@tanzaniaparks.go.tz

Facebook: [ismila_stoneagesite](https://www.facebook.com/ismila_stoneagesite)

Instagram: [ismila_stoneagesite](https://www.instagram.com/ismila_stoneagesite)

Website: www.tanzaniaparks.go.tz